

## **MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01 – 10 FEBRUARY, 2019 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 FEBRUARY, 2019.**

### **1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 01 – 10 FEBRUARY, 2019.**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilipelekea kuendelea kusukumwa kwa ukanda wa mvua (ITCZ) kuelekea kusini hadi kufika katika nchi yetu. Joto la bahari la juu ya wastani lilishuhudiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi hali hiyo iliyosababisha kutokea kwa vimbunga vilivyojulikana kwa majina ya Funani na Gelena mashariki mwa Madagascar ambavyo vilisababisha ongezeko la mvua katika maeneo ya kusini mwa nchi yetu na upepo mkali na mawimbi makubwa katika ukanda wote wa pwani. Kwa upande mwingine, joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani lilishuhudiwa eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ilipelekea kuvuma kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka magharibi ilipo misitu ya Congo.

### **1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01 –10 FEBRUARY, 2019**

Kuwepo kwa ukanda wa mvua ndani ya nchi yetu na vimbunga mashariki mwa Madagascar kulisababisha ongezeko la mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo ya kusini mwa nchi na kuongezeka kwa upepo mkali na mawimbi makubwa katika ukanda wote wa pwani.

## **2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11 - 20 FEBRUARI, 2019.**

### **2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 11 - 20 FEBRUARI, 2019.**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kubaki kusini katika nchi yetu. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi hali inayotarajiwa kusababisha kutokea kwa mgandamizo mdogo wa hewa katika rasi ya Msumbiji ambayo itaweza kusababisha ongezeko la mvua katika maeneo ya kusini mwa nchi yetu. Joto la bahari la wastani hadi chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kupelekea upepo kuvuma kutoka magharibi hivyo kuimarisha mifumo ya mvua katika maeneo mengi ya nchi.

### **2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE (11 - 20 FEBRUARI, 2019.)**

**Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Mvua katika maeneo machache.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Mvua nyepesi katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Mvua zinazoambatana na ngurumo pamoja na vipindi vifupi vya upepo mkali katika maeneo machache.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo pamoja na vipindi vifupi vya upepo mkali.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo pamoja na vipindi vifupi vya upepo mkali.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo pamoja na vipindi vifupi vya upepo mkali

Imetolewa na; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**